Kinga ya Moto

Nyumba za ghorofa



Kalmar kommun
BRANDKÅREN

Kinga ya Moto

Kengele ya moto

Kengele ya moto inaongeza uwezekano wa kutoka ndani ya nyumba pale inapoanza kuungua na moto. Kengele ya moto inaweza kuwekwa kwenye dari nje kidogo ya chumba cha kulala. Ukiwa umechomeka vifaa mbalimbali katika umeme chumbani, mfano simu ni vem ana kuwa na kengele ya moto chumbani. Kunatakiwa kuwe na kengele ya moto katika kila ghorofa. Ikiwa nyumba ina ukubwa zaidi ya 60 m^2 ni vema kuwa na kengele za moto zaidi ya mbili. Ni wajibu wako kama mwenye nyumba/mpangaji kuhakisha kwamba betri kwenye hizo kengele .Je hakuna kengele ya moto ndani ya nyumba yako? Tafadhali wasiliana na wamiliki wa nyumba ili wakupatie kengele za moto.

Jinsi ya kuhakikisha kengele za moto zinafanya kazi:

Bonyeza kitufe kinachopatikana kwenye kila kengele za moto. Kaa umekibonyeza kwa sekunde kadhaa. Isipoanza kupiga kelele jaribu kubadili betri. Fanya hivi mara kwa mara haswa kama ulikuwa umesafiri. Usisahau kuisafisha mara kwa mara.

Kumbuka kufanya majaribio kama kengele ya moto inafanya kazi.

Ili kuboresha ufanisi wa kengele ya moto mtandao wa ”Aktiv” una ofa kutuma ujumbe wa SMA kukumbusha kufanya majaribio ya kengele ya moto. Ingia katika tovuti yao www.skyddadigmotbrand.se ambapo unaweza kuona au kuchagua ni mara ngapi unataka wakutumie ujumbe wa SMS.

”Extinguishers” (kizimia moto cha mkono)

Idara ya zimamoto inashauri kwa kila mtu japo awe na kizimia moto chenye uzito wa 6 kg kwenye nyumba yake ikiwa na uwezo wa 43A 233 BC. Nyumba ”Sommarstugan” inahesabika kama nyumba ya kuishi. Kwenye magari, ”caravan” boti na vinavofanania inashauriwa kuwepo na kizimia moto chenye uzito wa 2 kg. Kizimia moto cha mkononi vinapatikana maduka makubwa (köpcentrum) maduka ya vifaa vya kuzimia moto

Blanketi la kuzima moto:

Ni vema kuwa na blanketi la kuzimia moto nyumbani. Unaweza kulitumia kuzimia moto kwenye nguo na kwenye moto ambao sio mkubwa na pia husaidia kuzuia moto kusambaa.

Timer na jiko:

Ni rahisi kusahau kuzima jiko na vyanzo vingi vya moto huanzia kwenye jiko. Kumbuka kuzima jiko kila mara ukitoka ndani ya nyumba au jikoni. Usiache vitu kwenye jiko na hakikisha kila mara kwamba jiko limizimwa likiwa halitumiki. Unaweza kununua Timer ambazo hujizima baada ya muda ulioweka. Spisvakt huzima jiko pale ambapo jiko linapoanza kupata lisilo la kawaida. Spisvakt huwekwa na mwenye nyumba.

Foto:
Johan Eklund

Jinsi ya kutumia kizimia moto cha mkono.

Elekeza kizimia moto kwenye moto.

Bonyeza chini kishikio.

Ongeza usalama wako na majirani zako.

Kila mwaka hutokea ajali za moto 32 katika nyumba katika eneo la zimamoto la Kalmar. Fuata maelekezo yafuatayo kuhakikisha nailinda nyumba yako na moto. Kama una maswali yeyote unakaribishwa kuwasiliana na kitengo cha zimamoto kwa namba 0480-45 75 10.

Zuia moto kwa kufunya ifuatavyo

- Weka vibiriti mbali na watoto.
- Usiwashe mashine ya kuoshea vyombo , mashine za kufulia, mashine ya kukaushia nguo kama haupo nyumbani au unapoenda kulala.
- Mafuta huanza kuungua vikipata moto mwingi. Ukipika na mafuta (kukaanga) jitahidi kuwa natahadhari kwamba inaweza kuanza kuungua. Usitumie maji kuzima moto!
- Chakula kilichoongua mara nyingi huwa ni sababu ya moto kuanza katika nyumba. Safisha ”filter” mara kwa mara kutoa mafuta.
- Usiache mishumaa inayowaka. Kumbuka kuzima mishumaa na usiache mishumaa inayowaka sehemu ambayo hamjakaa, mfano chumbani. Usiweke mapambo kwenye mishumaa ambayo yanaweza sababisha kuungua.
- Usiweke vitu ambavyo vinaweza sababisha moto kwenye ”balcony” yako.
- Usitumie waya za umeme ambazo zimeharibika kama unachomeka simu au kompyuta.
- Chomoa waya zote kwa mfano kwenye mashine ya kahawa ua birika ya kuchemshia maji wakati havitumik.
- Usivuti sigara kitandani au sehemu yeyote unayoweza kupitiwa na usingizi.

Uwe na mpango wa kujiokoa

- Ni sheria ya nchi kwamba kila nyumba lazima iwe na kengelea ya moto japo moto kwa kila nyumba. Badilisha betri mara kwa mara.
- Unashauriwa kuwa na kifaa cha kuzimia moto chenye uzito wa 6 kg.
- Usiweke vitu kwenye korido au ngazi ambavyo vinaweza kukuzuia wakati wa kutoka kama nyumba ikianza kuungua.

Kama nyumba ikianza kuungua... ⟶

Kama nyumba ikianza kuungua...

OKOA

... ndani ya nyumba yako:
Jaribu kuuzima moto. Kama umeshindwa funga mlango wa chumba ambapo moto unatokea na jaribu kutoka katika nyumba. Kama chumba kimejaa moshi – tambaa chini ya moshi kwa kuwa kwenye skafu mara nyingi huwa kuna hewa safi zaidi. Kama unashindwa kwenda kwenye mlango wa kutokea nenda kwenye kibaraza (balcony) au fungua dirisha na piga kelele za kuomba msaada. Usitumie ”Lifti” wakati wakujiokoa kutoka kwenye moto.

... kama ni kwa jirani:
Kama kuna moshi kwenye ngazi – baki ndani ya nyumba yako mpka zimamoto ije au piga simu na kutoa taarifa. Nyumba imejengwa kuzuia moshi kwa muda kati ya dk 30 mpaka 60. Wakati huo zimamoto inaweza kuuzima mot ona pia kukusaidia wewe kutoka kwenye nyumba.

TAHADHARI

Watahadhari wengine walio karibu ila na wao wakae katika usalama. Jitahidi kuongea kwa utulivu ili uswaogopeshe wengine. Fikiria kwamba watoto huwa wanapenda kujificha chini ya kitanda au makabatini.

TOA TAARIFA

Wewe na familia yako mkishakuwa salama piga simu namba 112. Toa maelezo ya haraka na sahihi na ueleze ni wapi unapigia simu(mtaa au anuani) na jina lako.

ZIMA

Kwanza jaribu kuzima moto mwenyewe ila usijaribu kufanya zaidi ya unavoweza! Zima chini yaani moto unapowaka na sio kwa juu. Usimwagie kwenye sehemu ambazo kuna waya za umeme. Kama ni sifuria inaungua jaribu kuweka mfuniko usitumie maji! Kama ni TV ianungua chomoa waya zote najaribu kuzima na kizimia moto au kwa kuimwagia maji.

Taarifa na maelekezo haya yameandaliwa na ”Räddningstjänsten” Storgöteborg na kurekebishwa na kikosi cha zimamoto cha Kalmar.

Kalmar Brandkår
Box 150, 391 21 Kalmar

Anuani ya ofisi	Kaggensgatan 39
Simu	0480-45 75 10
Fax	0480-45 75 00
Baruapepe	raddning@kalmar.se
Tovuti	www.kalmar.se/brand